BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA NA MASHIRIKA (LAAC) KUHUSU UWASILISHAJI WA RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI, KWA SERIKALI ZA MITAA NA MASHIRIKA KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Azza wa Jalla kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa wazima na wenye afya njema katika kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa na wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) Kuhusu Uwasilishaji wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Serikali kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, pia, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa kuweza kuwasilisha Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi wa mwezi wa Septemba, 2022 badala ya kuwasilisha katika Mkutano wa Baraza unaohusiana na mambo ya bajeti kama ilivyozoweleka.

Mheshimiwa Spika, shukurani za pekee zimfikie Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Watendaji wake wote wa Ofisi hiyo kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ya kufuatilia fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii kwa mashirikiano yao wanayonipatia wakati wote wa kazi za Kamati ikiwa ni pamoja na wakati wa kuzipitia, kuzichambua na kuzijadili taarifa hizi muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kutupa nguvu ili tuweze kutekeleza vyema majukumu tuliyopewa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwataja kwa majina Wajumbe na Makatibu wa Kamati ya LAAC kama ifuatavyo:-

Na	Jina	Uwakilishi	Nafasi
1.	Mhe. Habib Ali Mohammed	Mwakilishi, Jimbo la Mtambwe	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	Mwakilishi, Jimbo la Dimani	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Bakar Hamad Bakar	Mwakilishi, Jimbo la Wawi	Mjumbe
4.	Mhe. Haji Shaaban Wazir	Mwakilishi, Jimbo la Uzini	Mjumbe
5.	Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mwakilishi, Nafasi Maalum za Wanawake	Mjumbe
6.	Mhe. Shadya Mohammed Suleiman	Mwakilishi, Nafasi Maalum za Wanawake	Mjumbe
7.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	Afisa, Baraza la Wawakilishi Zanzibar	Katibu
8.	Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi	Afisa, Baraza la Wawakilishi Zanzibar	Katibu

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha Ripoti za Ukaguzi mbele ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kinaudhihirishia umma kuwa Ofisi hii inatekeleza vyema majukumu yake kama Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC baada ya kuzipitia Ripoti hizo imebaini kuwa makisio ya bajeti ya baadhi Taasisi hayatoi uhalisia unaoendana na vyanzo vyao vya mapato jambo hili husababisha ama makisio kuwa makubwa ukilinganisha na uhalisia wa vyanzo vyao au makisio kuwa makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo Kamati ya LAAC inaishauri Taasisi inayohusika na masuala ya kupanga mapato kuvijua vyanzo vyote vya mapato vya Taasisi husika kwa lengo la kuweza kupima vizuri uwezo wa vyanzo hivyo kabla ya kufanya makisio ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inashauri hili kwa kuwa zipo baadhi ya Taasisi zikifanya makadirio ya mapato hazikadirii kwa kuanzia na mwaka uliopita isipokuwa kwamba inakadiria chini zaidi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Kamati ya LAAC inasikitisha sana kuona baadhi ya Taasisi Mama ambazo ndio jicho la nchi hii katika kukuza mapato yake bado zinapata Hati Isiyoridhisha. Taasisi zenyewe ni Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA).

Mheshimiwa Spika, pamoja na Taasisi hizo kupata Hati Isiyoridhisha, hata hivyo, Ripoti ya Mdhibiti bado imetuweka njia panda kwani haikubainisha moja kwa moja ni Hati gani hasa Taasisi mbili hizi zimepata?. Mheshimiwa Spika, tumediriki kusema hivyo kwa kuwa katika Ripoti zilizokuwepo mbele yetu zimeeleza kuwa Hati Isiyoridhisha inajumuisha Hati tatu kama zifuatavyo:

i. Hati Yenye Shaka;

ii. Hati Mbaya; na

iii. Kushindwa Kutoa Maoni

hivyo, kwa upande wa Taasisi hizi tumeshindwa kutatua kitendawili hicho ambacho ni muhimu kuteguliwa kwa maslahi ya Baraza lako na nchi yetu kwa ujumla kwa kuwa Taasisi hizi zimeelezwa tu kiujumla kuwa zimepata Hati Isiyoridhisha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inashauku ya kujua jambo hilo hasa ikizingatiwa kuwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea za SMZ ya mwaka wa fedha 2020/2021 katika ukurasa wa 179, Mamlaka ya Uwanja wa Ndege imeelezwa kuwa imepunguza matumizi kwa asilimia 61.8 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2019/2020 lakini bado watendaji wa Mamlaka wameshindwa kusimamia vyema rasilimali fedha jambo lililompelekea Mdhibiti kubaini kuwa taarifa za fedha kwa kiasi kikubwa zina makosa na kwa ujumla wake hazikufuata viwango vinavyokubalika vya uandaaji wa taarifa za fedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC iliamini kuwa kitendo cha Mamlaka kupunguza matumizi ya fedha kingepelekea kwa kiasi kikubwa Mamlaka hii kupata Hati Inayoridhisha na kuiondoshea Mamlaka sifa mbaya iliyoikabili tokea mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Kamati ya LAAC iliona kuna utofauti wa tafsiri kwa baadhi ya Hati pamoja na majina ya Hati zilizotolewa na Ofisi hii katika Ripoti zilizopo mbele yetu na zile Ripoti za miaka ya nyuma. Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC kupitia Baraza hili inaomba kujua utofauti huo umetokana na mabadiliko ya ukaguzi duniani au Ofisi hii imegundua kuwa kulikuwa na makosa katika tafsiri na majina ya Hati hizo hapo kabla ndio maana katika Ripoti hizi mpya kuna utofauti huo?

Mheshimiwa Spika, kiujumla Kamati ya LAAC inayapongeza Mashirika, Taasisi Zinazojitegemea za SMZ na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuwasilisha kwa wakati

Hesabu za Mwisho wa Mwaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, Kamati ya LAAC imebaini kuwa bado zipo baadhi ya Taasisi zinafunga Hesabu za Mwisho wa Mwaka na kutoyajumuisha mambo mengine muhimu ambayo yanapaswa kuingizwa au kuonekana katika Hesabu hiyo ili kupata sura halisi ya hesabu ya Taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, endapo Kamati yako itabaini kasoro kama hizo basi utetezi mkubwa unaotolewa na Watendaji hao ni kuwa kasoro hiyo imefanywa kutokana na makosa au mapungufu ya kibinadamu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inaelewa kuwa hakuna mkamilifu katika matendo yetu isipokuwa Allah (Subhana Huwa Taala), hata hivyo, tunawaomba Watendaji kuzidi kuwa makini katika kutekeleza majukumu yao ili kuepusha kasoro za kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu pia tunaomba kuutoa kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwani Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka huwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha lakini bado Taarifa hizo zinaonekana zina upungufu wakati zisharidhiwa na Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ripoti ya Ukaguzi kwa Hesabu za Serikali za Mitaa, Kamati ya LAAC imebaini kuwa bado wananchi hawanufaiki kwa kiasi kikubwa na mapato yanayotokana na Serikali za Mitaa, kitendo hiki kinarejesha nyuma dhamira nzuri ya Serikali ya kuanzisha mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, jadweli linalofuata linathibitisha kauli yetu hiyo:

Nam.	Jina la Taasisi	Asilimia iliyokusanywa	Asilimia iliyopatikana kwa kazi za maendeleo
1.	Baraza la Manispaa Mjini	88	45.04
2.	Baraza la Manispaa Magharibi “A”	106	38
3.	Baraza la Manispaa Magharibi “B”	98	37
4.	Baraza la Mji Wilaya ya Kati	105.7	475
5.	Baraza la Mji Wilaya ya Kusini	103	52

6.	Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini “A”	100.152	16
7.	Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini “B”	47.66	26.43
8.	Baraza la Mji Chake Chake	109	25.05
9.	Baraza la Mji Mkoani	105	87.18
10.	Baraza la Mji Wete	121.32	69.5
11.	Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni	112.61	93.02

Mheshimiwa Spika, kutokana na kasoro hiyo Kamati ya LAAC inazitaka Serikali za Mitaa kuzidisha juhudi katika kukusanya mapato kwa lengo la kuwapatia maendeleo wananchi hasa ikizingatiwa kuwa hivi sasa Serikali za Mitaa hazina tena jukumu la kuwalipa mishahara Waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, ukiliangalia kwa kina Jadweli nililoliwasilisha utabaini kuwa asilimia kubwa ya Serikali za Mitaa zimekusanya mapato yake ya ndani kwa kiwango kinachoridhisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuridhisha huko, bado kuna baadhi ya vianzio vya mapato ambavyo mapato yake yanakusanywa au yanasimamiwa na Serikali Kuu na hakuna fedha yoyote inayopatikana kutoka katika vianzio hivyo na kwa vile vianzio ambavyo fedha zake zinapatikana basi upatikanaji wake ni wa kusuasua.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri wa mapato ambayo yanasimamiwa na Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ni kianzio cha mapato kinachotokana na minara ya simu ambapo katika kianzio hiki Kamati yako ilibaini kuwa Serikali za Mitaa hazijapatiwa hata senti moja tangu Wizara husika ilivyofunga mkataba na Kampuni ya ZICTIA mnamo mwezi wa Februari, 2021.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha endapo Serikali za Mitaa zitafuatilia suala hilo katika Kampuni husika huelezwa kwamba hazina mamlaka ya kufanya hivyo kwa kuwa hazikuingia mkataba wa moja kwa moja na Kampuni hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inaiomba Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kulifuatilia kwa karibu suala hili ili Mamlaka za Serikali za Mitaa ziweze kukusanya mapato hayo bila ya usumbufu wowote.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Kamati ya LAAC imebaini kuwa baadhi ya hoja zinazopata Mashirika, Taasisi Zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinachangiwa na Serikali Kuu kwa upande mmoja kwa kuwaamulia baadhi ya mambo ambayo utekelezaji wake unavunja Sheria, Kanuni na uratatibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Kamati ya LAAC inaiomba Serikali Kuu kuhakikisha kuwa inatoa ushauri kwa Taasisi zilizopo chini yake kama Sheria, Kanuni na uratatibu unavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inaipongeza Serikali katika jitihada zake za kuendeleza matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika Mawizara, Idara Mashirika ya Umma na Taasisi zake mbalimbali kwa lengo la kuleta ufanisi, uwazi, uwajibikaji pamoja na kuzuia mianya ya upotevu wa mapato ili Serikali iweze kufikia malengo yake na kuweza kuboresha hali za wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC imesikitishwa sana na kitendo cha baadhi ya Taasisi za Umma kuendelea kufanya ununuzi wa mifumo ya TEHAMA bila ya kufanya utafiti wa kutosha wa mifumo hiyo. Kitendo hicho kinapelekea mifumo hiyo kukabiliwa na changamoto nyingi ndani ya muda mfupi na hatimae kukosa ufanisi katika kufanya kazi kwake.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo inaitia hasara kubwa Serikali kwa kutumia fedha nyingi za wavuja jasho wa nchi hii bila ya mafanikio yoyote wakati kuna shughuli nyingi za maendeleo zinahitaji kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa IFMs unaotumiwa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango bado unakabiliwa na changamoto kadhaa jambo ambalo linarudisha nyuma uwajibikaji, ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa na mfumo huo licha ya kwamba Serikali inaendelea kutumia fedha nyingi katika kuuhudumia mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, huduma zinazotolewa kwa ajili kuugharamia mfumo huo ni pamoja na kuulipia leseni kila mwaka, kufanyiwa matengenezo “Services level”, kulipia moduli wakati miongoni mwa moduli hizo hazifanyiwi kazi na badala yake kazi zinazostahili kufanywa katika moduli hizo zinafanywa nje ya mfumo kwa njia ya “manually”.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri wa moduli ambayo haijawahi kutumiwa kabisa katika Mfumo wa IFMs ni Moduli ya Usimamizi wa Mali na Vifaa Ghalani (Asset and Inventory Managment) na badala yake Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango imenunua mfumo mwengine kwa ajili ya kazi hiyo wakati Mfumo wa IFMs pia unaruhusu kufanyika kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inazidi kusisitiza kuwa, hayo ni matumizi mabaya ya fedha za umma na inaishauri Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuufanyia

marekebisho haraka iwezekanavyo Mfumo wa IFMs ili kuondoa dosari mbali mbali zilizobainika na Mkaguzi Mkuu na hatimae Mfumo huo kuweza kutumika kikamilifu na kuepusha Serikali kuingia katika gharama zisizo za lazima kwa kuendelea kununua mifumo ambayo inafanya kazi sawa na moduli ambazo zinapatikana katika Mfumo wa IFMs.

Mheshimiwa Spika, Mifumo hii ya TEHAMA ndio tegemeo kubwa katika kutunza taarifa na nyaraka mbalimbali za Taasisi na Serikali kwa ujumla, wakati mwengine taaarifa huwa ni siri na zenye umuhimu mkubwa kwa taasisi ambapo huenda zikaathiri utendaji kazi wa Taasisi endapo taarifa hizo zitapotea kutokana na kukosekana udhibiti imara wa usalama wa kimtandao.

Mheshimiwa Spika, Ripoti imeeleza kuwa baadhi ya Taasisi za Umaa hazina kabisa maafisa usalama TEHAMA na kwa baadhi ya Taasisi za Umma ambazo maafisa hao wapo basi hawana taaluma ya kutosha katika utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa viwango na sera za TEHAMA zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inahofu kubwa juu usalama wa utumiaji wa mifumo yetu ya TEHAMA kutokana changamoto mbalimbali ikiwemo ya ukosefu wa elimu pamoja na wataalamu wa usalama wa mifumo hiyo. Hivyo basi, Kamati ya LAAC inashauri Serikali kuwa, kwa kuwa inaweka mikakati madhubuti ya kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika Taasisi zake ni vyema uhamasishaji huu uende sambamba na kuwapatia mafunzo maafisa TEHAMA katika maeneo mbalimbali hususan katika udhibiti wa usalama wa mifumo ya TEHAMA ambapo mifumo hii imebeba nyaraka na taarifa mbalimbali za Serikali ambazo zikipotea au kuharibiwa na Programu haribifu zitaleta hasara kubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LACC inaishauri Serikali kuzitumia taasisi zake zinazohusika na masuala ya Mifumo ya TEHAMA kama vile Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA (ZICTIA) pamoja na Wakala wa Serikali Mtandao (e-Government Zanzibar) wakati wa mchakato wa kutafuta mifumo ili kupata mifumo sahihi na yenye tija.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Kamati ya LAAC inaunga mkono ushauri uliotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa ni muhimu kwa Taasisi za Umma kufuata miongozo inayotolewa na Wakala wa Serikali Mtandao (e-Government) katika kusimamia vyema uwajibikaji wa mifumo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kiujumla Kamati ya LAAC imezipokea na kuzifanyia kazi Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa upande wa Mashirika, Taasisi za Umma na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na hatimae kuwasilisha Ripoti yake kama Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020 zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumalizia naomba kugusia mambo mawili muhimu kama

ifuatavyo :

Mheshimiwa Spika, Moja, pamoja na shukurani tulizozitoa kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, tunaiomba Ofisi hiyo wakati inatekeleza majukumu yake kuhakikisha kuwa inafuata misingi yote ya ukaguzi ili kuepusha malalamiko yasiyokuwa na lazima.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inashauri hili kwa kuwa iliwahi kupata malalamiko kwa Taasisi zinazokaguliwa kuwa baadhi ya Wakaguzi wamekuwa wanatekeleza majukumu yao wakiwa tayari na majibu hasi juu ya Taasisi fulani jambo linalopelekea Mkaguzi huyo kutokutaka mashirikiano ya karibu na Wakaguliwa na hatimae kuandika hoja ambazo zina majibu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na malalamiko hayo, Kamati ya LAAC inaiomba tena Ofisi ya Mdhibiti kutekeleza shughuli zake kwa mujibu wa taratibu zilizopo na kamwe isiwe tayari kunyooshewa vidole.

Mheshimiwa Spika, Pili, Kamati ya LAAC haipingani na kauli ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi juu ya Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) kuzichukulia hatua haraka iwezekanavyo tuhuma mbali mbali zilizoelezwa kwenye Ripoti za Ukaguzi, isipokuwa kwamba, Kamati ya LAAC inazitaka Taasisi zote kuhakikisha kuwa endapo nyaraka zimechukuliwa na ZAECA mara tu Taasisi hiyo itakavyopokea barua ya kazi kutoka katika Kamati hii kuwasiliana na ZAECA haraka iwezekanavyo kwa lengo la kurejeshewa nyaraka hizo ili kila chombo kinachohusika kiweze kutekeleza jukumu lake bila ya usumbufu wowote na shughuli ya Kamati ikimalizika nyaraka hizo zitarudishwa tena ZAECA kwa hatua zao.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inatoa indhari hiyo kwani zipo baadhi ya Taasisi nyaraka zao zilichukuliwa na ZAECA na Kamati yako ilipata usumbufu wa kuzipata nyaraka hizo wakati ilivyozihitaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba kuwashukuru Wajumbe wa Baraza hili, kwa utulivu wao na kwa kunisikiliza kwa makini wakati wote nilipokuwa nawasilisha maoni ya Kamati ya LAAC kuhusiana na Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa upande wa Mashirika, Taasisi za Umma na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, pia, nawaomba Wajumbe wako waitumie haki yao ya msingi iliyotolewa na kanuni ya 43(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi ya kumuuliza maswali Mheshimiwa Waziri husika juu ya Ripoti hizi kwa lengo la kupata ufafanuzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.



…….

Habib Ali Mohammed,
Mwenyekiti,
Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC),
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.